**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MAADHIMISHO YA SIKU YA AFYA YA MACHO

**DODOMA: 09 Oktoba, 2025**

Tanzania inaungana na mataifa mengine Duniani kuadhimisha **Siku ya Afya ya Macho Duniani (World Sight Day),** tukio hili muhimu la kimataifa lilianzishwa mwaka 1998 na Lions Club International Foundation, Shirika la Afya Duniani (WHO), pamoja na Muungano wa Mashirika ya Kimataifa ya Huduma za Macho (IAPB). Lengo la siku hii ni kuhamasisha utekelezaji wa Dira ya Kimataifa ya Kutokomeza Upofu Unaozuilika na kuhimiza upatikanaji wa haki ya kuona kwa wote.

Maadhimisho haya hufanyika kila mwaka Alhamisi ya pili ya mwezi Oktoba, ambapo dunia huungana kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuchukua hatua dhidi ya upofu na upungufu wa kuona unaoweza kuzuilika. Mwaka 2025, maadhimisho haya yamebeba kaulimbiu ***"Penda Macho Yako, Simulizi Yako ni Mwanga kwa Mwingine."***

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), takribani watu milioni 450 duniani wanakabiliwa na matatizo ya uoni yanayohitaji tiba, huku wengi wao wakishindwa kupata huduma kutokana na gharama kubwa au upungufu wa miundombinu. Tafiti zinaonyesha kuwa mtoto mmoja kati ya watoto 1,000 ana ulemavu wa kutokuona, na watoto katika nchi zenye uchumi wa chini na wa kati wako katika hatari mara mbili hadi tano zaidi ya kushindwa kuhudhuria shule kutokana na matatizo ya macho. Hali hii inasababisha changamoto kubwa katika elimu, ajira, na ushiriki wa kijamii kwa watoto na vijana wengi ulimwenguni.

Hapa nchini Tanzania, inakadiriwa kuwa takriban watu milioni 12 wanahitaji huduma za afya ya macho. Magonjwa yanayoongoza ni pamoja na mtoto wa jicho (cataract), upeo mdogo wa macho kuona mbali au karibu unaorekebishika kwa miwani (refractive errors), shinikizo la macho (glaucoma), madhara ya ugonjwa wa kisukari kwenye pazia la jicho (diabetic retinopathy), pamoja na mzio na maambukizi ya macho. Magonjwa haya yanarudisha nyuma maendeleo ya familia, jamii na Taifa kwa ujumla.

Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2024, jumla ya watu milioni 1.5 walihudumiwa kwenye kliniki za macho nchini, ambapo asilimia 42 walikuwa watoto chini ya miaka 15. Kati ya watoto hao, asilimia 6.3 walifika wakiwa tayari na ulemavu wa kutokuona.

Kwa mwaka 2025 jumla ya huduma mkoba 59 zimefanyika katika maeneo mbali mbali nchini ambapo jumla ya wananchi 132,107 wamefikiwa na kupatiwa huduma katika maeneo yao wanayoishi, aidha Katika kipindi cha miaka mitano Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeimarisha huduma za macho katika hospitali za kanda na taifa, mwaka 2024 pekee zaidi ya watoto 1,000 walifanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho na kupatiwa miwani, sawa na asilimia 55.6 ya wahitaji waliolengwa.

Vyanzo vikuu vya matatizo haya ni pamoja na mzio, upeo mdogo wa macho, majeraha ya macho, mtoto wa jicho, makengeza, makovu kwenye kioo cha jicho, ugonjwa wa surua, upungufu wa vitamini A na saratani ya macho (retinoblastoma). Hali hii inaonesha umuhimu wa kufanya uchunguzi wa macho mapema na kuchukua hatua za kinga ili kuzuia upofu unaoweza kuzuilika.

Wizara ya Afya inatoa wito kwa jamii kuhakikisha afya ya macho inapewa kipaumbele katika maisha ya kila siku na kuhimiza wananchi kufanya uchunguzi wa macho angalau mara moja kwa mwaka na kuzingatia ushauri wa wataalamu wa afya. Aidha, nawaapongeza wadau na watumishi wa sekta ya afya kwa mchango wao katika kutoa huduma za macho na elimu ya kinga.

Afya ya macho ni nguzo muhimu ya maendeleo. Penda macho yako, kwa sababu simulizi yako inaweza kuwa mwanga kwa mwingine. Tukichukua hatua leo, tutaokoa vizazi vijavyo dhidi ya ulemavu wa kutokuona unaozuilika.

Imetolewa na:

**Dkt. Grace Magembe**
**MGANGA MKUU WA SERIKALI**